SHERIA YA UKIMWI TANZANIA

Sheria ya Ukimwi yaani "**THE HIV AND AIDS (PREVENTION AND CONTROL) ACT, 2008"** ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania tarehe 1 Februari, 2008. Tarehe 4 Aprili, 2008, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Sheria hii ni mahususi kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI, kuendeleza na kutunza afya ya jamii kuhusiana na virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Sheria hii pia inatoa mwongozo wa huduma inayotakiwa kwa watu walio ambukizwa au kwa wale waliokatika hatari ya kupata maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa kutumia rasilimali zilizopo.

WAJIBU WA JUMLA KWA TUME YA TAIFA YA KUDHIBITI UKIMWI

Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) ina wajibu wa kuratibu shughuli zote za UKIMWI nchini. Kwa mujibu wa sheria hii kila mtu, kitengo, shirika, serikali, dini, viongozi wa Kimila pamoja na waajiri katika vitengo binafsi ambao wanafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria ya Ukimwi wana wajibu wa kushirikiana na kuwasiliana na Tume ili kuhakikisha kuwa rasilimali zinagawanywa kwa usawa na hivyo kuzuia ugawaji wa rasilimali hizo kwa kiasi

kikubwa katika eneo moja au kwenye sekta moja. Vilevile kuanzisha shughuli zinazolenga kuzuia na kudhibiti VVU na UKIMWI. Mipango yote ya Wizara, Vitengo, Taasisi za Serikali, Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kiraia na Sekta mbalimbali inatakiwa kuwasilishwa TACAIDS kwa ajili ya usimamizi na ushauri zaidi kabla ya kuanza kutekelezwa.

WAJIBU WA SERIKALI, WATU BINAFSI NA TAASISI MBALIMBALI

- Wajibu wa kuchukua hatua za hali ya juu za usalama kuhakikisha inapunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI na ugonjwa wa UKIMWI.

- Wajibu wa kuandaa au kutengeneza vipindi vinavyotoa elimu inayopinga unyanyapaa pamoja na ubaguzi kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Vilevile Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ina wajibu wa kuratibu vipindi vitakavyokuwa vinafundisha jinsi ya kuwatunza wagonjwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Taarifa au elimu hiyo itatoka kwa muundo na teknolojia inayotakiwa na ipatikane kwa watu wote, hasa wale wasiojiweza

- Kila mwajiri akishirikiana na wizara ya afya ana wajibu wa kuanzisha na kusimamia programu maalum katika sehemu ya kazi kwa ajili ya waajiriwa. Programu hiyo itahusisha elimu ya UKIMWI, ugawaji wa kondomu pamoja na kuwajali na kuwasaidia wale wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

- Watoa huduma za afya kila wanapofanya upasuaji au matibabu ya meno na utabibu mwingine unaofanana na huduma hizo wana wajibu wa kuwa mwangalifu katika kutunza na kutupa ama kuteketeza sindano zilizotumika na vifaa vilivyotumika kwenye upimaji wa damu au uchafu mwingine wowote wa mtu anayeaminika kuwa ameathirika na virusi vya UKIMWI.

- Kila shirika au taasisi inayojishughulisha na masuala ya VVU/UKIMWI kwa kushirikiana na serikali za mitaa, itawajibika kutoa kwa wanajamii wa eneo linalowazunguka huduma za afya, uangalizi na faraja zinazohusu virusi vya UKIMWI na UKIMWI pia kuwasaidia watoto wasiojiweza na kuhakikisha yatima wanapatiwa huduma muhimu.

- Vituo vinavyotoa huduma ya afya vina wajibu wa kuhakikisha kuwa vinasimamia, kufuatilia na kutoa tiba pamoja na huduma zote zinazotakiwa ili kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

- Kituo cha huduma au bima ya afya, iwe ya umma au binafsi, kina wajibu wa kutoa huduma za afya kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI bila ubaguzi wowote.

HAKI ZA MTU ANAYEISHI NA VVU

- Kupata huduma za afya ya mwili na akili kwa kadri ya ubora unaohitajika.
- Kupata matibabu sahihi ya magonjwa nyemelezi.
- Kupata haki zote alizo nazo binadamu mwingine yeyote ambaye ajaathirika.

WAJIBU WA MTU ANAYEISHI NA VVU

- Kulinda wengine wasipate maambukizi ya VVU.
- Kushiriki na kuchangia katika maendeleo ya kisayansi na mafanikio yake.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- Serikali, viongozi wa siasa, dini na wa kimila pamoja na wafanyakazi wa sekta binafsi wawe mbele katika kupiga vita ubaguzi kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi.(s.4(2))
- Hamna mtu yeyote ambaye atalazimishwa kupima kama ana virusi vya ukimwi pasipo hiari yake (s.15(3))
- Wizara ya Afya itahakikisha kuwa ARV pamoja na huduma nyingine muhimu za afya na dawa zinapatikana. (s.24(2))
- Mtu yeyote haruhusiwi kumbagua au kumnyanyasa kwa aina yeyote mtu mwenye VVU au anayehisiwa kuwa na VVU.
- Mtoto atapimwa tu pale patakapokuwepo kibali cha kuridhia kwa maandishi kutoka kwa mzazi au mlezi.

MAKOSA NA ADHABU AMBAZO ZIMEAINISHWA KATIKA VIFUNGU VYA 21 (3), 32, 35 , 46 NA 47.

- Kushindwa kumfahamisha mwenzi au mtu ambaye una mahusiano naye ya kimapenzi kuwa una virusi vya UKIMWI na pia kuchutochukua hatua mutambuka ya kutoeneza maambukizi husika.
- Kumnyanyapaa au kumnyanyasa kwa maneno au vitendo mwenzi wako au mtu ambaye una mahusiano naye ya kimapenzi kwasababu ana virusi vya UKIMWI.
- Kumnyima mtu mwenye virusi vya UKIMWI haki zake za msingi kama, kutompa huduma za afya, kumkatalia kusafiri, kumnyima makazi, kumnyima kazi au chochote ambacho kina chembechembe za ubaguzi.
- Taasisi zote zinazotoa huduma kwa waathirika wa UKIMWI kwa kutumia fedha za misaada kushindwa kufikisha misaada hiyo kwa wahusika.
- Mtaalamu wa afya au mtu yeyote anayehusika na upimaji kutoa siri ya hali ya kiafya kuhusiana na majibu ya vipimo vya UKIMWI ya mtu yeyote.
- Kuwa na nia ovu ya kusambaza kwa makusudi virusi vya UKIMWI.

KANUNI ZILIZOPITISHWA KISHERIA KWA UFUPI

- Watoa nasaha lazima wawe wamepata mafunzo maalum ya kufanya kazi hiyo.
- Mtu yeyote anayetaka kupima VVU lazima apewe nasaha (counselling) kabla na baada ya kupima/kupimwa.

- Upimaji wa VVU ni wa hiari.
- Kujaza fomu ya kuridhia kupimwa VVU.
- Baada ya upimaji, majibu yatatolewa kwa maandishi au kwa mdomo na pale mtu atakapokuwa na VVU ataelezwa haki zake, ikiwa ni pamoja na kutonyanyaswa kwa aina yeyote na mtu yeyote.
- Pale mtu anapokuwa hajitambui au hawezi kutoa ridhaa ya kupimwa VVU na daktari au mtoa huduma ya afya anaona ni muhimu kufanya hivyo, basi mtu huyo atapimwa bila ridhaa yake.
- Utunzaji wa siri kwa upande wa watoa huduma za afya.
- Upatikanaji na utunzaji mzuri wa dawa (ARV) na nyingine zinazohusiana na ugonjwa wa UKIMWI ambazo pia zina ubora unaokubalika.
- Watoa huduma kuwa makini na kazi zao wanapohudumia wagonjwa ili kuzuia maambukizi.

MWISHO

Naamini kwa kiasi kikubwa kuwa sheria hii ikitekelezwa itasaidia kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI.